



Tina na baba yake, walikuwa wamekaa nje.

Tina alitazama juu. Aliona nyota zinametameta.

Alimuuliza baba, "baba nyota ziko kama vipepeo?" Baba alisema, hapana.



Ni za ajabu, zinametameta na kumulikamulika.
Lo, nazitamani sana.

Tina alisema, "Baba, baba, ninazitamani nyota.
Utaninunulia?" Baba alicheka.



Aaa Tina, nyota haziuzwi zinakaa huko juu tu.

Tina aliuliza, "utaenda kunichukulia?" Baba alijibu, "Subiri kidogo Tina, nitakutafutia."


Aaa! Ijumaa iko karibu na Jumamosi, si eti baba ee! Naam, baba alisema, ni kweli, Ijumaa na Jumamosi ni siku zinazofuatana.



Tina alikaa kimya.

Kisha alisema kuwa, akiwa mkubwa atakwenda kuzifuata.

Wote wakacheka na kuingia ndani.



Tina alikuwa anacheza.

Mara, alitokea malaika. Malaika alimetameta kama zile nyota.

Tina alitabasamu akauliza, "Na mimi naweza kuwa malaika?" Malaika alicheka.



Malaika alimwambia Tina, " Wewe ni mtoto mdadisi, unataka nini?" Tina alisema, "Ninapenda nyota, zinavutia. Ninazitamani, zinametameta na ninafurahi ninapozitazama."
Malaika alisema," Nitakupa mabawa." Malaika alimgusa Tina mgongoni, mara, Tina alipata mabawa. Tina alifurahi sana. Malaika naye alifurahi, kisha alitoweka.



Tina alipaza sauti alisema, "Siwezi kwenda peke yangu kuchuma nyota. "

Aliziambai nyota," Enyi nyota nakuja kuwachukua. Nyota zilimsikia, zilimulikamulika zaidi.



Njiwa alipita, alimsikia Tina akiziita nyota akamwendea.

Njiwa alimuuliza unaongea na nyota? Tina akajibu, ndiyo.

Natafuta rafiki wa kwenda naye.



Tina na njiwa walianza kupaa.

Walipaa, walipaa juu, juu zaidi.

Kwenye mlango wa mbingu, walimkuta babu mlinzi.

Wakamuomba waingie.



Babu akasema, "Atakayeweza kulijibu swali hili ataingia."

"Nyota moja ukiongeza nyota nne unapata nyota ngapi?"

"Unapata nyota tano." Tina alijibu haraka.




Tina hufanya bidii shuleni. Alipenda masomo hasa ya hisabati na kusoma. Babu alifurahi sana akamwambia, "Umepata, kila mmoja akachukue nyota tano."

Tina na njiwa kila mmoja alichagua nyota kubwa tano. Tina alisema, "Nitampa baba, mama, kaka na rafiki yangu Fatuma, kila mmoja nyota moja."



Kumbe, Tina alikuwa kwenye ndoto. Uso wake ulionyesha tabasamu. Mkono mmoja alikunja ngumi, Bila shaka alibeba nyota zile tano.



Tina, alicheka kwa sauti.
Wazazi wake walienda
chumbani kwa Tina.
Walimtazama mtoto wao.
Mama alimbusu usoni.



Baada ya juma moja. Baba alinunua mfano wa nyota tano kubwa. Zilikuwa na taa ndogondogo.

Usiku zilipowashwa, zilikuwa zinametameta na kutoa mwanga mzuri.

Tina alifurahi sana. Aliziweka mbili kwenye chumba chake.

